

# Pima Kadi ya Jamii

## Shiriki Kuboresha Mifumo ya Afya

**Halmashauri ya Mji wa Kibaha**

**Pwani**

Sikika

**Oktoba, 2020**

## Kuhusu Sikika na Wadau

Sikika kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ufadhili wa Global Fund kupitia asasi ya Benjamin Mkapa Foundation (BMAF) imetekeleza mradi wa Pima Kadi ya Jamii kwa lengo la kuimarisha mifumo ya afya na mwitikio wa jamii katika Halmashauri ya mji wa Kibaha. Lengo kuu likiwa kuboresha huduma za VVU na UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria, na utayari wa Jamii katika kukabiliana na dharura na maafa.

## Yaliyomo


Kuhusu Sikika na Wadau....................i

Yaliyomo....................ii

Orodha ya Vifupisho....................iv

Shukrani....................v

Muhtasari....................vi

Sehemu ya Kwanza....................1

1.0. Utangulizi....................1

1.1. Mbinu za Utekelezaji....................1

Sehemu ya Pili....................4

2.0 Matokeo na Mjadala....................4

2.1. Utangulizi....................4

2.2. VVU/UKIMWI....................4

2.2.1. Uhaba wa majengo na vyumba vya kutolea huduma za VVU/UKIMWI....................4

2.2.2. Upungufu wa dawa za kufubaza makali ya VVU kwa miezi mitatu....................4

2.2.3. Uhaba wa dawa za magonjwa nyemelezi kwa WAVIU....................5

2.3. Kifua Kikuu....................6

2.3.1. Ukosefu wa kipimo cha Kifua Kikuu katika baadhi ya vituo....................6

2.3.2. Uhaba wa vyumba maalumu kwa ajili ya huduma za Kifua Kikuu....................7

2.3.3 Uhaba wa dawa za kupunguza makali ya dawa za Kifua Kikuu....................7

2.4. Malaria....................7

2.4.1. Kipimo cha Malaria kibadilishwe kiletwe cha Hadubini....................7

2.4.2. Jamii ipokee maagizo ya watoa huduma kulingana na miongozo....................8

2.4.3. Mafunzo kwa watoa huduma....................9

2.5. Mwitikio wa Jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa....................9

2.5.1. Uelewa mdogo kwa baadhi ya wananchi juu ya magonjwa ya dharura na maafa....................9

2.5.2. Uhaba wa vitendea kazi vya kukabiliana na maafa na dharura vituoni....................9

2.6. Mifumo shirikishi ya Jamii....................10

2.6.1. Wahuduma wa Afya ngazi ya Jamii (WAJA)....................10

2.6.1.1. Ukosefu wa vitendea kazi kwa baadhi ya WAJA....................10

2.6.1.2. Uchache wa WAJA kwa baadhi ya mitaa....................10

2.6.1.3. Baadhi ya WAJA kukosa elimu na mafunzo ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali na maafa ..... 11
2.6.2. Wajumbe wa kamati za vituo ..... 11
Sehemu ya Tatu ..... 13
3.0. Hitimisho na Mapendekezo ..... 13
3.1. Hitimisho ..... 13
3.2 Mapendekezo ..... 13
Viambatanisho ..... 14
Kiambatanisho Na 1: Mpango Kazi ..... 14
Kiambatanisho Na 2: Orodha ya washiriki ..... 22

## Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| **ARV** | Antiretroviral (Dawa za Kufubaza Makali ya Virusi vya UKIMWI) |
| **CHF** | Community Health Fund (Bima ya Afya ya Jamii) |
| **CHMT** | Council Health Management Team (Timu ya Usimamizi ya Afya ya Halmashauri) |
| **RHMT** | Regional Health Management Team (Timu ya Usimamizi ya Afya ya Mkoa) |
| **TB** | Tuberculosis (Kifua Kikuu) |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |
| **WAJA** | Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii |
| **WAVIU** | Watu waishio na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI |

## Shukrani

Natoa shukrani za dhati kwa ushirikiano tuliopata kutoka kwa uongozi wa Mkoa wa Pwani na Halmashauri ya Mji wa Kibaha hususani, Mkurugenzi Mtendaji na Mganga Mkuu wa Halmashauri. Kipekee tunawashukuru Mganda mkuu wa Halmashauri, Katibu wa Afya, Mratibu wa UKIMWI pamoja na timu nzima ya uendeshaji wa huduma za afya ya halmashauri ya Mji Kibaha.

Pia, tunawashukuru watoa huduma, wapokea huduma pamoja na wadau wa afya kutoka katika kata na vituo 6 ambao walishirikiana nasi katika kufanikisha utekelezaji wa zoezi hili.

Mwisho, tunatambua na kuthamini maoni, ushauri na maazimio yaliyofikiwa kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya katika halmashauri ya Mji Kibaha hususani katika maeneo ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na utayari wa jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa.

Asanteni,

**Irenei Kiria,**
**Mkurugenzi Mtendaji**

## Muhtasari

Utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Afya na Mwitikio wa Jamii katika utoaji wa huduma za afya kwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha umelenga kukuza ushiriki wa jamii katika kuboresha utoaji wa huduma za VVU/UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria pamoja na utayari wa jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa.

Kwa kutumia njia ya Pima Kadi ya Jamii, mradi ulihusisha mafunzo kwa washiriki 198 kati yao 87 ni wanaume na 111 ni wanawake kuhusu miongozo ya utoaji wa huduma za VVU/UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria pamoja na utayari wa jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa. Tathimini ya upatikanaji wa huduma hizo ilifanyika kupitia maoni ya washiriki katika mijadala 14 iliyoendeshwa kwa njia ya vikundi vyenye uwakilishi kutoka katika makundi ya wananchi, watoa huduma za afya ngazi ya jamii (WAJA), wajumbe wa kamati za afya za vituo, viongozi wa kijamii na watoa huduma za afya katika ngazi ya kituo. Washiriki walitoka katika kata sita (6) zenye vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo ni, Kituo cha afya Mkoani, Zahanati ya Kongowe, Mwendapole, Misugusugu, Vikawe na Visiga. Tathimini hiyo iliwezesha washiriki kuainisha mafanikio yaliyofikiwa vituoni na changamoto zinazokabili utoaji wa huduma hizo.

Baadhi ya mafanikio yaliyoainishwa ni pamoja na huduma za VVU/UKIMWI kutolewa vituoni ikiwemo upimaji, utoaji wa dawa za kufubaza VVU na ushauri nasaha, uwepo wa kamati za kudhibiti maambukizi ya VVU katika ngazi ya mtaa, kata na Halmashauri, uwepo wa WAJA kwa baadhi ya mitaa ambao wamesaidia uibuaji wa wagonjwa wa TB na UKIMWI. Huduma za kifua kikuu zinaendelea vema, baadhi ya vituo vinatoa huduma ya upimaji na hakuna uhaba isipokuwa wa dawa mwambata. Kwa upande wa Malaria, utoaji wa elimu kuhusu Malaria vituoni unaendelea, ugawaji wa vyandarua vyenye dawa kwa walengwa ikiwemo wamama wajawazito. Pia Halmashauri imefanikiwa kuunda kamati za maafa kuanzia ngazi ya mtaa kwa lengo la kukabiliana na maafa mara yanapotokea.

Hata hivyo, masuala kadhaa yalibainishwa kama changamoto zinazohitaji kuboreshwa vituoni. Miongoni mwa changamoto hizo ni uhaba wa majengo/vyumba vya kutolea huduma za VVU/UKIMWI vituoni, jamii kutokuwa na imani na baadhi ya vipimo vya Malaria, ukosefu wa vipimo vya Kifua Kikuu kwa baadhi ya vituo na ufahamu mdogo kwa baadhi ya wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa. Baada ya kuanisha changamoto wadau wa afya waliandaa mpango kazi kwa ajili ya utekelezaji.

## Sehemu ya Kwanza

### 1.0. Utangulizi

Halmashauri ya Mji wa Kibaha ni miongoni mwa Halmashauri 9 za Mkoa wa Pwani ambayo inaundwa na tarafa mbili (2) za Kibaha na Kongowe, Kata kumi na nne (14) na Mitaa sabini na tatu (73). Kwa mujibu wa takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Mji wa Kibaha unakadiriwa kuwa na idadi ya wakazi 144,241 kati yao 70,334 ni wanaume na wanawake ni 73,906 ambao hutegemea huduma za afya kutoka katika vituo 33 vya kutolea huduma za afya vilivyopo katika halmashauri, kati ya hivyo, vituo 17 ni vya Serikali na 16 ni vya binafsi. Vituo 20 hutoa huduma ya upimaji wa virusi vya UKIMWI wakati 17 kati ya hivyo hutoa huduma ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na 13 hutoa huduma ya tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na maaambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Katika vituo vilivyopo Halmashauri ya Mji wa Kibaha vituo 10 vinatoa huduma ya upimaji wa kifua Kikuu na vituo 23 ndio vinatoa huduma ya dawa za kifua Kikuu[1]. Aidha, kwa upande wa Malaria, hali ya maambukizi ya ugonjwa wa Malaria katika halmashauri ya Mji wa Kibaha imeonesha kuwa na kiwango cha chini cha wastani wa asilimia 0.8 ikilinganishwa na wastani wa mkoa wa Pwani wa asilimia 5.3.

Jumla ya watu 198 kati yao wanaume 87 (44%) na wanawake 111 (56%) walishiriki katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi ambapo kundi la watumia huduma za kinga na matibabu ya UKIMWI, Kifua Kikuu na malaria ni themanini (80), WAJA arobaini na tatu (43), wajumbe wa kamati za vituo ishirini na nane (28), viongozi wa serikali za mitaa ni kumi na tano (15) watoa huduma vituoni kumi na nane (18), CHMT kumi na tatu (13) na RHMT ni mmoja (1). Wadau kutoka katika makundi haya walishirikishwa kutokana na umuhimu wao katika kuhakikisha huduma za afya katika maeneo ya VVU/UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa zinaboreshwa katika halmashauri.

### 1.1. Mbinu za Utekelezaji

Utekelezaji wa mradi umezingatia hatua zote nane (8) za Pima Kadi ya Jamii kama zifuatazo; (i) Kutambulisha Mradi, (ii) kuchagua washiriki na vituo vya kutolea huduma za afya, (iii) mafunzo kwa washiriki, (iv) kuandaa vipaumbele vya wapokea huduma (v) kuandaa vipaumbele vya watoa huduma, (vi) kuandaa mpango kazi, (vii) kuwasilisha na kuidhinisha mpango kazi kwa wadau na (viii) ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji.

[1] Ofisi ya Mganga Mkuu, 2020

## 1. Kutambulisha Mradi

Mradi ulitambulishwa katika ngazi mbalimbali za serikali na jamii ukianzia Wizara za Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kisha ngazi ya Mkoa na halmashauri ya Mji wa Kibaha. Vilevile, utambulisho ulifanyika kwa wadau wa afya ikiwemo; wananchi, wajumbe wa kamati za afya za vituo, watoa huduma za afya ngazi ya jamii, viongozi wa kijamii, watoa huduma ngazi ya kituo na timu ya usimamizi wa afya ya Halmashauri (CHMT).

## 2. Kuchagua Washiriki na Vituo vya kutolea Huduma za Afya

Kwa kuzingatia maeneo mahususi ya mradi, washiriki walichaguliwa kulingana na uwakilishi wa makundi mbalimbali ikihusisha Kundi la watu wenye ulemavu, Watu waishio na Virusi vya Ukimwi (WAVIU), Wagonjwa wa Kifua Kikuu wa zamani na sasa, Wanawake, akinamama wajawazito, Vijana, Watoa huduma za afya ngazi ya Jamii (WAJA), Wajumbe wa Kamati za Vituo, Viongozi wa Jamii (MEO/WEO) pamoja na Watoa huduma ngazi ya kituo. Upatikanaji wa vituo vya kutolea huduma za afya ulifanyika kwa kuzingatia; (1) Uwakilishi wa Kituo cha Afya na Zahanati (2) Uwakilishi wa eneo la mjini na vijijini (3) Utoaji wa huduma za maeneo mahususi ya mradi.

## 3. Mafunzo kwa Washiriki

Mafunzo kuhusu dhana ya Pima Kadi na miongozo ya utoaji wa huduma za afya (standard of care) yalitolewa katika makundi tajwa hapo juu. Mafunzo hayo yalitolewa kwa kuzingatia maeneo mahususi ya mradi (VVU/UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na utayari wa jamii katika kukabiliana na dharura na maafa) kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya katika maeneo hayo.

## 4. Kuandaa Vipaumbele vya Wapokea Huduma

Baada ya mafunzo kutolewa, washiriki walipata fursa ya kujadili na kubainisha mafanikio na changamoto katika utoaji wa huduma za afya vituoni katika maeneo ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na magonjwa ya dharura na maafa. Aidha, wapokea huduma walibainisha mahitaji kwa vituo, kupitia vikundi vya mjadala na kisha walibainisha vipaumbele vya mahitaji kwa kupigia kura mahitaji hayo kulingana na umuhimu.

5. **Kuandaa Vipaumbele vya Watoa Huduma**

Kupitia vikundi vya mjadala watoa huduma kwa pamoja walibainisha mahitaji yao na kisha kuweka vipaumbele vya mahitaji hayo kwa kupigia kura mahitaji kulingana na umuhimu.

6. **Kuandaa Mpango Kazi**

Katika hatua hii, mahitaji ya makundi mbalimbali yaliwasilishwa na kujadiliwa katika kikao cha ndani kilichohusisha timu ya usimamizi ya shughuli za Afya ya Halmashauri, wawakilishi wa wapokea huduma na watoa huduma, ambapo rasimu ya mpango kazi iliandaliwa kwa ajili ya kuidhinishwa na wadau wa afya.

7. **Kuwasilisha na Kuidhinisha Mpango Kazi kwa Wadau**

Katika hatua hii, wadau wa afya waliidhinisha rasimu ya mpango kazi kwa ajili ya utekelezaji. Mkutano wa wadau ulihusisha wawakilishi kutoka katika makundi mbalimbali tajwa hapo juu, pamoja na mwakilishi kutoka ofisi ya Mkurugezi pamoja na timu ya usimamizi wa afya ya Mkoa.

8. **Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji**

Hatua hii hutekelezwa kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango kazi ulioidhinishwa na wadau wa afya. Ufuatiliaji hufanyika mara moja kwa mwezi na mkutano wa tathmini hufanyika baada ya miezi mitatu (3) ili kujadili utekelezaji wa mpango kazi.

# Sehemu ya Pili

## 2.0 Matokeo na Mjadala

### 2.1. Utangulizi

Sehemu hii inaonesha masuala yatokanayo na majadiliano ya vikundi ambayo yalijumuishwa na kuchambuliwa kwa kuainisha na kulinganisha taarifa ama maoni ya washiriki kutoka katika makundi yote sita (6). Mahitaji yaliyobainishwa yalijadiliwa na kupatiwa ufafanuzi na kuwekewa maazimio kwa ajili ya utekelezaji. Mtiririko umegawanywa katika maeneo 4 ambayo ni; 1. VVU/UKIMWI, 2. Kifua Kikuu, 3. Malaria, 4. Mwitikio wa jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa na mifumo shirikishi ya Jamii.

### 2.2. VVU/UKIMWI

Halmashauri ya Mji wa Kibaha imeendelea kuhakikisha huduma za VVU/UKIMWI zinatolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo upimaji, ushauri nasaha na utoaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU (ARV) kuanzia ngazi ya Zahanati. Sambamba na jitihada hizi, halmashauri imeendelea kuhakikisha kuwa kamati za kudhibiti maambukizi ya VVU zinakuwepo kuanzia ngazi ya mtaa.

Hata hivyo, pamoja na jitihada tajwa bado kuna changamoto zinazorudisha nyuma utoaji wa huduma za VVU/UKIMWI vituoni. Baadhi ya changamoto hizo ni;

#### 2.2.1. Uhaba wa majengo na vyumba vya kutolea huduma za VVU/UKIMWI

Maoni ya wapokea huduma yameonesha kuwa vituo 4 (Zahanati ya Mwendapole, Misugusugu, Vikawe na Kituo cha afya Mkoani) kati ya 6 vilivyoshiriki vina changamoto ya uhaba wa majengo kwa ajili ya huduma za VVU/UKIMWI ambayo husababisha kukosekana kwa usiri wakati huduma za afya zinapotolewa vituoni. Changamoto hii ilithibitishwa na watoa huduma za afya vituoni kwa kubainisha uhaba na ukosefu wa majengo/vyumba vya kutolea huduma za VVU/UKIMWI. Wadau waliazimia kuwa jamii ihamasishwe kujitolea rasilimali katika kufanikisha ujenzi wa majengo vituoni. Aidha, ili kutatua changamoto hii *"vituo viingize kwenye bajeti mahitaji ya ujenzi na vipeleke mahitaji hayo ngazi ya kata/WADC, pia wananchi na wadau wahamasishwe kushiriki katika ujenzi wa majengo"* Pendekezo kutoka kwa idara ya usimamizi wa huduma za afya ya Halmashauri.

#### 2.2.2. Upungufu wa dawa za kufubaza makali ya VVU kwa miezi mitatu

Watoa huduma katika vituo 4 (Kituo cha afya mkoani, zahanati ya Kongowe, Misugusugu, na Mwendapole) kati ya 6 walibainisha uwepo wa changamoto ya uhaba wa dawa za kufabaza

makali ya VVU kwa mtindo wa kutoa dozi ya muda wa miezi mitatu mitatu ambapo hupelekea wapokea huduma kukosa dawa hizi muhimu kulingana na mwongozo. Maoni yalionesha kuwa kwa sasa wapokea huduma hupatiwa dawa za ARV kwa muda wa mwezi mmoja badala ya miezi mitatu kwa lengo la kuwawezesha wapokea huduma wengi kupata dawa hizo. Mapendekezo ya kutatua changamoto hii yalitolewa vituo kujumuisha mahitaji ya dawa kwenye bajeti. *"Tunaelekea kipindi cha kuandaa bajeti vituo viandae bajeti na kuweka mahitaji ya dawa za ARV kama kipaumbele kulingana na mahitaji ya vituo"* alisema mjumbe wa idara ya usimamizi wa huduma za afya ya Halmashauri.



***Picha No. 1:*** *Afisa Tathmini wa Halmashauri Ndugu Mashaka Juma akifafanua jambo katika kikao wa wadau.*

### 2.2.3. Uhaba wa dawa za magonjwa nyemelezi kwa WAVIU

Watoa huduma kutoka katika vituo viwili (Zahanati ya Vikawe na Visiga) kati ya 6 walibainisha kuwa kumekuwa na upungufu wa dawa za Co-trimoxazole, Fluconazole na Nystatin vituoni ambazo ni muhimu kwa magonjwa nyemelezi yanayowapata WAVIU. Aidha, Kituo cha Misugusugu walibainisha kuwa kumekuwa na uhaba wa dawa za Septrine pekee. Hii imepelekea wagonjwa kuathirika na magonjwa nyemelezi mfano Fangasi. Ili kutatua changamoto hii watoa huduma walipendekeza kuwa *mteja mwenye Bima ya afya anapokosa dawa kwenye kituo kimoja anaweza kwenda kwenye kituo kingine kutafuta dawa hizo zinatolewa kulingana na mwongozo na si kwa matakwa ya mtu.*

### 2.3. Kifua Kikuu

Kwa upande wa Kifua Kikuu, baadhi ya vituo vinatoa huduma kama vile upimaji wa sampuli (makohozi) pamoja na utoaji wa dawa kwa wagonjwa wenye maambukizi. Vilevile, uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu umefanyika kupitia WAJA kwa kufuatilia, kuwatambua na kuwapa elimu kuhusu umuhimu wa kuanza kutumia dawa mapema.

Hata hivyo, katika halmashauri ya Mji Kibaha baadhi ya changamoto zilibainika kuwa ni vikwazo katika jitihada za utoaji wa huduma za Kifua Kikuu vituoni. Changamoto hizo ni kama vile;

#### 2.3.1. Ukosefu wa kipimo cha Kifua Kikuu katika baadhi ya vituo

Zahanati ya Misugusugu na Visiga kati ya vituo 6 havina kipimo cha uchunguzi wa kifua kikuu na hivyo hulazimika kuchukua sampuli ya Makohozi na kusafirisha kwa ajili ya uchunguzi katika Kituo cha afya Mkoani, Seminari na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tumbi. Hivyo kupelekea ucheleweshaji katika utoaji wa huduma za vipimo kwa haraka vituoni. Maoni yameonesha kuwa ili kutatua changamoto hii "wananchi wapewe elimu kuwa vituo vya Misugusugu na Visiga havitoi huduma ya upimaji badala yake sampuli huchukuliwa na kusafirishwa kwenye vituo vya Mkoani, Seminari na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tumbi" alisema Mjumbe wa idara ya usimamizi wa huduma za afya ya Halmashauri.



***Picha No. 2:*** *Mratibu wa Kifua Kikuu Halmashauri ya Mji wa Kibaha akifafanua jambo katika mkutano wa wadau uliofanyika katika halmashauri ya Mji Kibaha.*

### 2.3.2. Uhaba wa vyumba maalumu kwa ajili ya huduma za Kifua Kikuu

Changamoto ya uhaba wa vyumba maalum vya kutolea huduma za Kifua Kikuu ilibainishwa na wapokea huduma kutoka Zahanati ya Mwendapole ambapo wagonjwa wa kifua kikuu huchanganywa na wagonjwa wengine. Hali hii hupekelea wagonjwa wasiokuwa na kifua kikuu kuwa katika hatari ya kupata maambukizi. Ili kutatua changamoto hii ilipendekezwa kuwa jamii ihamasishwe kujitolea rasilimali kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa majengo. Aidha, vituo viingize kwenye bajeti hitaji la ujenzi wa majengo pamoja na kutafuta wadau ambao watafanikisha ujenzi wa majengo hayo.

### 2.3.3 Uhaba wa dawa za kupunguza makali ya dawa za Kifua Kikuu

Wapokea huduma kutoka katika katika kituo 1 (Zahanati ya Kongowe) katika ya vituo 6 walibainisha kuwa kumekuwa na uhaba wa dawa za kupunguza makali ya dawa za kifua kikuu kama vile; Vitamin B Complex na Pyridoxine (Vitamin B6) ambazo hupunguza madhara ya ganzi kwenye mikono na miguu ambayo hujitokeza kwa baadhi ya wagonjwa. Utatuzi wa changamoto hii ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kujiunga na Bima ya Afya ya Jamii (CHF) ili kuweza kupata dawa za kupunguza makali ya dawa za hizo. Aidha, vituo vilishauriwa vinunue dawa kama Vitamin B Complex ambazo zitatolewa kupitia mfuko wa bima ya afya ya jamii (CHF).

### 2.4. Malaria

Kwa upande wa Malaria, halmashauri imefanya jitihada mbalimbali katika kuendeleza mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria kwa kuhakikisha vituo kuanzia ngazi ya Zahanati vinatoa huduma za Malaria kama vile vipimo na dawa. Aidha, watoa huduma wameendelea kutoa elimu katika vituo vya afya kuhusu ugonjwa wa Malaria na namna ya kujikinga. Vilevile, jitihada za kugundua mazalia ya mbu katika halmashauri zimefanyika na kisha kupulizia dawa katika mazalia yaliyobainika. Vyandarua vyenye dawa vimesambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwafikia walengwa wakiwemo wanawake wajawazito. Katika muktadha huo, wanawake wajawazito wamepatiwa kinga ya Malaria bure hali ambayo imesaidia kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa Malaria kwa wanawake wajawazito na kupelekea kutokuwepo kwa vifo vya wanawake wajawazito vinavyosababishwa na ugonjwa wa Malaria.

Hata hivyo, katika utekelezaji wa mradi baadhi ya changamoto zimebainika kurudisha nyuma jitihada za kupambana na Malaria vituoni. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo;

### 2.4.1. Kipimo cha Malaria kibadilishwe kiletwe cha Hadubini

Wapokea huduma kutoka katika kituo cha Afya Mkoani walibainisha kuwa kipimo cha Malaria cha MRDT kinachotumika kituoni hakifanyi kazi vizuri na hivyo hupelekea hofu ya majibu ya kipimo kutokuwa sahihi. Maoni yameonesha kuwa wapokea huduma wanahitaji kipimo cha

Hadubini kitakachotumika kwa ajili ya upimaji badala ya kipimo kilichopo sasa. Mapendekezo yalitolewa kuwa, elimu itolewe kwa wananchi kuhusu utendaji mzuri wa kipimo kilichopo cha MRDT ili kuondoa dhana potofu ya watumia huduma kutokuamini kipimo hicho. Aidha, jamii ipewe elimu kuwa "sio kila homa ni malaria" alisema Mjumbe kutoka idara ya usimamizi wa huduma za afya ya Halmashauri.

### 2.4.2. Jamii ipokee maagizo ya watoa huduma kulingana na miongozo

Watoa huduma wameendelea kutoa elimu katika vituo vya afya kuhusu ugonjwa wa Malaria na namna ya kujikinga. Hata hivyo, ilibainika kuwa wapokea huduma hawazingatii maagizo yanayotolewa na watoa huduma kuhusu utumiaji wa dawa za Malaria ambazo hutolewa kwa mujibu wa miongozo. Changamoto hii ilibainishwa na watoa huduma kutoka katika vituo 4; Zahanati za Kongowe, Mwendapole, Misugusugu na Kituo cha Afya Mkoani. Hii husababisha kutokuwa na maelewano baina ya watoa huduma na wapokea huduma. Ili kutatua changamoto hii, "*elimu iendelee kutolewa kwa jamii ili kuelimishwa juu ya umuhimu wa kusikiliza na kufuata maelekezo ya wataalam" alisema Mtoa huduma na kuongeza kuwa "dawa za Malaria hutolewa kulingana na mwongozo*".



***Picha No. 3:*** *Mganga mfawidhi wa Zahanati ya Misugusugu Ndugu. Salim Mohamed alifafanua jambo katika kikao kilichokutanisha wadau wa afya katika halmashauri ya Mji Kibaha.*

### 2.4.3. Mafunzo kwa watoa huduma

Watoa huduma kutoka katika vituo vya Vikawe na Visiga walibainisha hitaji la kupata mafunzo kulingana na wakati na miongozo mipya inayotolewa ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Ukosefu wa mafunzo kwa watoa huduma hupelekea kukosekana kwa ufanisi na ujuzi katika utoaji wa huduma za afya. Maoni yalionesha kuwa hitaji hili ni muhimu kufanyiwa kazi ili watoa huduma wapatiwe mafunzo endelevu kulingana na wakati na miongozo mipya.

### 2.5. Mwitikio wa Jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa

Kwa upande wa magonjwa ya dharura na maafa, kuna kamati maalum za maafa kwenye ngazi za mitaa zilizoundwa kwa lengo la kukabiliana na dharura na maafa pindi yanapojitokeza. Katika baadhi ya mitaa kamati hizi hazitekelezi majukumu yake. Changamoto hii huathiri utoaji wa elimu kuhusu huduma za dharura na maafa kwa wananchi. Ili kutatua changamoto hii ilipendekezwa kamati za maafa zilizopo zikumbushwe majukumu yao kwa kupatiwa elimu ya huduma za dharura na maafa. Vilevile, kamati ya maafa ya Wilaya imeweka mipango ya kufanya semina elekezi kwa kamati za mtaa juu ya namna ya kupambana na magonjwa ya dharura na maafa.

Hata hivyo, katika utekelezaji wa mradi ilibainika kuwa baadhi ya changamoto zinarudisha nyuma jitihada za kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa. Baadhi ya changamoto hizo ni;

### 2.5.1. Uelewa mdogo kwa baadhi ya wananchi juu ya magonjwa ya dharura na maafa

Wapokea huduma kutoka katika vituo 2 (Zahanati ya Misugusugu na Mwendapole) kati ya 6 walibainisha kuwa kuna uelewa mdogo kwa baadhi ya watumia huduma juu ya namna ya kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa. Hivyo, jamii inakosa ujuzi na mbinu muhimu za kuweza kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa pindi yanapojitokeza. Mapendekezo ya utatuzi wa changamoto hii ni kuhakikisha elimu inatolewa kwa wapokea huduma kuhusu namna ya kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa. Aidha, makundi maalumu katika jamii yapewe kipaumbele katika kupatiwa elimu ya magonjwa ya dharura na maafa. Sambamba na hilo, tathimini ifanyike juu ya uhai wa kamati za maafa zilizopo ngazi za mitaa ili kufahamu utendaji kazi wao ikiwemo utoaji wa elimu kwa jamii juu ya magonjwa ya dharura na maafa.

### 2.5.2. Uhaba wa vitendea kazi vya kukabiliana na maafa na dharura vituoni

Changamoto hii ilibainishwa na watoa huduma kutoka katika vituo 4 (Zahanati ya Kongowe, Mwendapole, Misugusugu na Kituo cha Afya Mkoani) ambavyo viko jirani na barabara kuu (ya magari ya mikoani). Ilielezwa kuwa, ukosefu wa vifaa huathiri utoaji wa huduma pindi maafa na dharura zinapojitokeza kama vile ajali za barabani. Ili kutatua changamoto hii ilipendekezwa kuwa vituo viongeze bajeti ya vifaa tiba na vitendea kazi ambavyo ni muhimu katika kukabilina na maafa/dharura zinazojitokeza. *"Tunaelekea kipindi cha kuandaa bajeti ni wakati mwafaka kila*

*kituo kuweka bajeti ya mahitaji ya vifaa tiba kwa ajili ya kukabiliana na maafa na dharura" alisema Mjumbe wa CHMT.*

## 2.6. Mifumo shirikishi ya Jamii

Kamati za usimamizi wa kituo, watoa huduma ngazi ya jamii, na viongozi wa jamii ni miongoni mwa mifumo shirikishi ya huduma za afya kwa jamii. Kila mtendaji wa mfumo ana wajibu na dhamana kwa wananchi katika kutoa na kusimamia upatikanaji wa huduma bora za UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, na pia muitikio jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharurua na maafa.

### 2.6.1. Wahuduma wa Afya ngazi ya Jamii (WAJA)

Watoa huduma za afya ngazi ya jamii wamekuwa ni kiungo kikubwa kati ya wapokea huduma na watoa huduma vituoni. Katika halmashauri kuna WAJA zaidi ya 200 ambao wanatoa huduma za afya kwa jamii katika mitaa ikiwemo kuibua wagonjwa wa UKIMWI na kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU. Pia, halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetoa mafunzo kwa WAJA katika maeneo mbalimbali ya afya ikiwemo VVU/UKIMWI na Kifua Kikuu. Pamoja na mafanikio tajwa baadhi ya changamoto zilizobainika kama vikwazo ambavyo vinazorudisha nyuma juhudi za WAJA katika kutekeleza majukumu yao ni;

#### 2.6.1.1. Ukosefu wa vitendea kazi kwa baadhi ya WAJA

Wapokea huduma kutoka katika vituo 4 (Zahanati ya Kongowe, Vikawe, Mwendapole na Visiga) kati ya 6 walibainisha kuwa WAJA hawana vitendea kazi muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao. Ukosefu wa vifaa hivyo hupelekea WAJA kufanya kazi zao katika mazingira magumu na hivyo wengi huvunjika moyo wa kujitolea. Baadhi ya vitendea kazi hivyo ni; vitambulisho vya kazi, usafiri, miamvuli, buti za mvua na mabegi. Ili kutatua changamoto hii ilipendekezwa kuwa wadau na wahisani washirikishwe na kuhamasishwa kutoa msaada ili WAJA waweze kupata vitendea kazi vitakavyowasaidia kutekeleza majukumu yao. Vitendea kazi ni moja ya motisha kwa WAJA na huongeza ufanisi wa wajibu wao kwa jamii. Aidha, ilipendekezwa kuwa wadau wanaotaka kufanya kazi na WAJA wanapaswa kupitia ngazi ya Halmashauri ili kupata maelezo zaidi juu ya mambo wanayoweza kuwawezesha WAJA katika kuboresha utendaji kazi wao.

#### 2.6.1.2. Uchache wa WAJA kwa baadhi ya mitaa

Halmashauri ina WAJA wanaotoa huduma za afya katika mitaa mbalimbali iliyopo katika halmashauri, hivyo kufanya uwepo wa wastani wa WAJA 2 kwa kila mtaa. Hata hivyo, changamoto ya uchache wa WAJA ilibainishwa na wapokea huduma kutoka katika vituo 3 (Zahanati ya Vikawe, Mwendapole, Misugusugu) kati ya vituo 6 vilivyoshiriki katika utelekelezaji wa mradi. Maoni haya ya wapokea huduma yalithibitishwa na watoa huduma kutoka katika

vituo vya Kongowe, Mwendapole, Misugusugu na Kituo cha afya Mkoani ambapo ilibainika kuwa idadi ya WAJA ni ndogo kwa baadhi ya mitaa, hivyo huathiri shughuli muhimu kama vile uibuaji wa wagonjwa wa UKIMWI na Kifua kikuu mitaani na utoaji wa elimu ya Bima ya afya kwa wananchi. Wadau waliazimia kuwa, *"hamasa itolewe kwa wananchi ili wajitolee kufanya kazi za WAJA katika mitaa wanayoishi"* alisema Mjumbe wa idara ya usimamizi wa huduma za afya ya Halmashauri. Aidha, iliazimiwa pia kuwa wadau mbalimbali wanaohitaji kufanya kazi na WAJA wawasiliane na halmashauri ili kupata taarifa na maelekezo ya namna bora ya kuwapata WAJA na kufanya nao kazi.

#### 2.6.1.3. Baadhi ya WAJA kukosa elimu na mafunzo ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali na maafa

Wapokea huduma kutoka katika vituo 3 (Zahanati ya Kongowe, Visiga na Kituo cha Afya Mkoani) kati ya 6 walibainisha kuwa baadhi ya WAJA hawana elimu na mafunzo katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali kama kifua kifua, UKIMWI, Ukoma, magonjwa ya mlipuko na maafa. Changamoto hii hupelekea WAJA kukosa ujuzi na mbinu muhimu za kukabiliana na changamoto hizo pindi zinapotokea. Mapendekezo ya kutatua changamoto hii yalitolewa na hivyo ilipendekezwa kuwa elimu ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali na maafa itolewe kwa WAJA ili kuwapatia ujuzi pamoja na kuongeza ufanisi katika utendaji wa majukumu yao.

### 2.6.2. Wajumbe wa kamati za vituo

Katika utekelezaji wa mradi iligundulika kuwa vituo vyote vina wajumbe wa kamati za afya za vituo ambao wanasaidia kufanikisha utekelezaji wa malengo na mipango ya kituo pamoja na kubuni vyanzo vya mapato vituoni. Hata hivyo, wadau walipendekeza uwepo wa mafunzo ya mara kwa mara kwa kamati hizi ili kuwawezesha wajumbe wa kamati ya afya ya kituo ikiwemo wajumbe wageni wanaojiunga na kamati kufanya kazi kwa ufanisi.

*"Mafunzo yatolewe kuhusu miongozo kwa wajumbe wa kamati za afya za vituo. Pia, wajumbe wa kamati wawasilishe maeneo ambayo wanahitaji kupatiwa mafunzo kwa walezi wa vituo ambao pia ni wajumbe wa* idara ya usimamizi wa huduma za afya ya Halmashauri", *alisema Mganga Mkuu wa Halmashauri.*



***Picha No. 4:*** *Mganga Mkuu wa Wilaya Dkt. Tulitweni Mwinuka akifafanua jambo katika mkutano uliokutanisha wadau wa afya.*

# Sehemu ya Tatu

## 3.0. Hitimisho na Mapendekezo

### 3.1. Hitimisho

Utekelezaji wa mradi wa kuimarisha mifumo ya afya na mwitikio wa jamii katika utoaji wa huduma za afya kwa halmashauri ya Mji wa Kibaha umetoa fursa kwa wapokea huduma, watoa huduma na wadau mbalimbali wa afya katika halmashauri kutathmini mafanikio na vilevile changamoto zinazorudisha nyuma utoaji wa huduma za afya katika maeneo ya UKIMWI, Kifua kikuu, Malaria pamoja na utayari wa jamii katika kukabiliana na magonjwa ya dharura na maafa. Ili kutatua changamoto zilizoainishwa na wadau wa afya kwa kushirikiana na Timu ya usimamizi wa afya ya Halmashauri waliandaa mpango kazi na kuweka maazimio ambayo yatasaidia kuboresha utoaji wa huduma za afya katika maeneo tajwa hapo juu kama unavyoonekana kwenye ukurasa wa 14 hadi 21 wa ripoti hii.

### 3.2 Mapendekezo

Uboreshaji wa mifumo ya kutolea huduma za UKIMWI, Kifua kikuu, malaria na mifumo ya dharura na maafa ni muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma zenye viwango kwa jamii. Hivyo, tunapendekeza;

- Jamii ihamasishwe kujiunga na Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa ili kupata huduma za afya zinazotolewa vituoni pamoja na kuimarisha hali ya mapato ya vituoni.
- Mazingira na miundombinu ya utoaji wa huduma za afya katika vituo yazingatie usiri ili kuhakikisha wapokea huduma wanapata huduma bora za afya zinazostahiki.
- Jamii ipewe elimu kuhusu huduma za afya zilizopo na zinazotolewa (kama vile upimaji, utoaji wa dawa, ushauri nasaha) vituoni. Pia, watoa huduma waendelee kupatiwa mafunzo kulingana na miongozo na mabadiliko yanayojitokeza.
- Vituo viboreshe mfumo wa utoaji huduma kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu ili kuepusha wagonjwa wengine kupata maambukizi.
- Jamii na watoa huduma wapatiwe elimu juu ya namna ya kujikinga na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na maafa.
- Jamii ipatiwe elimu na hamasa kushiriki katika masuala ya utoaji na usimamizi wa huduma za afya vituoni.

## Viambatanisho

***Kiambatanisho Na 1: Mpango Kazi***

| HUDUMA ZA VVU/UKIMWI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **No.** | **Mahitaji** | **Maazimio** | **Muhusika** | **Muda** |
| **1.** | Uhaba wa Majengo na vyumba vya kutolea huduma za VVU/UKIMWI (CTC & RCH) pamoja na Kifua Kikuu katika vituo vya Mwendapole, Misugusugu, Kituo cha afya Mkoani, Vikawe na Visiga | Kuhamasha jamii katika kushiriki na kujitolea katika ujenzi wa majengo. Kituo kiingize kwenye bajeti suala la ujenzi wa majengo. Pia, kutafuta wadau kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa majengo. | Mganga mfawidhi, wajumbe wa kamati ya kituo na wananchi. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **2.** | Uhaba wa dawa za magonjwa nyemelezi kwa WAVIU kama vile; Ceptrine, Co-trimoxazole, Fluconazole na Nystatin katika vituo vya Misugusugu, Vikawe na Visiga. | Dawa zipo ila elimu itolewe kwa wagonjwa kukosekana kwa muda haimaanishi hazipo kabisa. Aidha, Wananchi wapewe elimu ya kujiunga na Bima ya Afya (CHF) ili wapate huduma za ziada kama dawa za magonjwa mengine. Pia, elimu itolewe sio wagonjwa wote wanapaswa kupewa Septrine maana hutolewa kulingana na mwongozo. | Waganga wafawidhi, watoa huduma na WAJA | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **3.** | Upungufu wa dawa za kufubaza makali ya VVU kwa WAVIU kwa muda wa miezi mitatumitatu | Vituo viongeze bajeti ya mahitaji wakati wa kuomba ili dawa ziweze kupatikana kwa miezi mitatumitatu | Waganga wafawidhi na Halmashauri | Kuanzia Oktoba-Machi bajeti inapoandaliwa |
| **4.** | Hakuna vifaa tiba mfano, CD4 Mashine, HB Mashine, Microscope, Renal Function and Centrifuge Mashine | Kuomba wadau kusaidia upatikanaji wa vifaa tiba tajwa | Wadau, Halmashauri na waganga wafawidhi | Kuanzia Oktoba-Machi bajeti inapoandaliwa |
| **5.** | Waathirika/wagonjwa wa UKIMWI na Kifua kikuu kutofuata maelekezo ya wataalam katika ufuasi wa dawa eneo la | Elimu itolewe kwa wapokea huduma kufuata maelekezo na WAJA wapatiwe elimu ili waweze kuelimisha wananchi/jamii juu ya umuhimu wa kufuata maelekezo katika ufuasi wa dawa. | Watoa huduma WAJA na Wananchi | Kuanzia Novemba na kuendelea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kongowe. Mfano ARV na Dawa za Kifua kikuu. | | | |
| | **KIFUA KIKUU** | | | |
| **1.** | Ukosefu wa kipimo cha Kifua Kikuu (TB) katika Zahanati za Misugusugu na Visiga | Misugusugu na Visiga sio vituo kinachotumika kupima TB badala yake sampuli (makohozi) huchukuliwa na kutumwa Mkoani, Seminari na Tumbi kwa ajili ya vipimo. Hivyo, elimu itolewe kwamba vituo tajwa havipimi TB badala yake sampuli huchukuliwa na kusafirishwa kwa ajili ya uchunguzi. | Mganga Mfawidhi wa Kituo, Kamati ya kituo na Jamii | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **2.** | Uhaba wa dawa za kupunguza makali ya dawa za Kifua Kikuu (TB) katika zahanati ya Kongowe. | Kutoa elimu na kuhamasisha Wananchi wajiunge kwenye Bima ya Afya (CHF) kwa ajili ya kupata dawa za kupunguza makali ya dawa za TB. Aidha, vituo vinunue dawa kama Vitamin B Complex ambazo zitatolewa kupitia CHF. | Watoa huduma kwenye vituoni na WAJA | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **3.** | Ukosefu wa uelewa/elimu juu ya umuhimu wa upimaji wa TB na VVU mtaa kwa mtaa. Mfano Mwendapole katika Mitaa ya kwa Dude na kwa Balozi Daudi. | Elimu iendelee kutolewa kuanzia ngazi ya kituo. Kutumia matukio muhimu kama "TB day" ili kutoa elimu ya umuhimu wa kupima. Wataalamu pia waende mpaka kwenye makampuni mbalimbali kwa ajili ya ku-screen TB. Kuhamasisha jamii kupima kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. WAJA kutoa elimu ya TB pamoja na kufanya screening. Elimu itolewe juu ya "tambua TB" kupitia simu inayomwezesha mtu kufanya uchunguzi binafsi wa TB kwa kubonyeza ***152*05# Ok** | Halmashauri, WAJA, Watoa huduma, viongozi wa serikali ya mtaa | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| | **MALARIA** | | | |
| **1.** | Jamii iwe tayari kupokea maagizo ya watoa huduma kulingana na mwongozo katika kutoa huduma. Mfano; Mwongozo unaeleza dawa ya malaria ambayo | Elimu iendelee kutolewa kwa jamii ili kueleweshwa juu ya umuhimu wa kusikiliza maelekezo ya mtoa huduma/mtaalam. | WAJA, Watoa huduma, wajumbe wa kamati za afya za kituo | Kuanzia Novemba na kuendelea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | mgonjwa anapaswa kupewa lakini wagonjwa wanakataa na kuchagua dawa wanazopenda. | | | |
| **2.** | Kipimo cha Malaria kibadilishwe kutoka MRDT kiletwe cha Hadubini (Kipimo hakitoi majibu sahihi) | Kutoa elimu zaidi kwa wananchi juu ya umuhimu/utendaji wa kipimo cha MRDT ili kuondoa dhana ya kuamini mhusika ana malaria. "Sio kila homa ni malaria". | Mganga Mfawidhi Mkoani, watoa huduma za afya na WAJA. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **3.** | Uhitaji wa mafunzo ya mara kwa mara kwa watoa huduma kulingana na wakati uliopo na miongozo mipya iliyopo mfano; Malaria, HIV, TB na maafa | Mafunzo yatolewe kwa watoa huduma kulingana na wakati na miongozo mipya | Halmashauri, watoa huduma na wadau | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| | **MWITIKIO WA JAMII KATIKA KUKABILIANA NA MAGONJWA YA DHARURA NA MAAFA** | | | |
| **1.** | Uelewa mdogo kwa baadhi ya wananchi juu ya namna ya kukabiliana na maafa pindi yanapojitokeza katika maeneo ya Misugusugu na Mwendapole Mfano, Mafuriko na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu. | Elimu iendelee kutolewa kwa wananchi juu ya namna ya kukabiliana na maafa. Makundi maalumu pia yapewe kipaumbele katika elimu ya maafa. Tathimini ifanyike juu ya uhai wa kamati za maafa kuanzia ngazi ya mtaa. Elimu iwe endelevu ambayo itasaidia hata watendaji wanaohama kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kupata elimu/ufahamu juu maafa. | Watoa huduma ngazi ya kituo, WAJA, Kamati za maafa kuanzia ngazi ya mitaa | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **2.** | Uhaba na Ukosefu wa vitendea kazi (vifaa) vya kukabiliana na maafa vituoni (Mfano Misugusugu) kama vile Vizima moto (Fire extinguisher) na vifaa vya kutoa huduma pale ajali za barabarani zinapojitokeza. | Kuongeza bajeti ya vifaa tiba. Vituo viandae bajeti ya uhitaji wa Vifaa tiba kwa mwaka ujao wa fedha (2021/22) na kupeleka Halmashauri. | Mganga mfawidhi, Wajumbe wa kamati ya Kituo | Kuanzia Mwezi wa Oktoba-Machi 2021 |
| **3.** | Baadhi ya kamati za maafa hazipo hai katika kutekeleza majukumu | Kamati za maafa zikumbushwe juu ya majukumu yao na kuwajibika kutoa elimu katika | Watendaji wa Mitaa na Kata, Halmashauri | Kuanzia Novemba na kuendelea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | yake. Mfano; Misugusugu na Visiga | jamii juu ya namna ya kukabiliana na maafa. | | |
| **4.** | Baadhi ya WAJA hawana elimu ya kutosha katika kukabiliana na maafa mfano Moto, mafuriko na magonjwa ya mlipuko kama Kipindupindu na magonjwa mengine kama Malaria, TB. Changamoto hii imeonekana Kituo cha afya Mkoani, zahanati ya Kongowe na Visiga | Elimu ya kukabiliana na maafa itolewe kwa WAJA pamoja na magonjwa ya mlipuko. | Wasimamizi wa WAJA, Watoa huduma za afya vituoni na WAJA | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| | **MENGINEYO** | | | |
| **1.** | Maudhi (lugha zisizofaa) hasa kwa wamama wajawazito pindi wanapohudhuria huduma za Kliniki katika Zahanati ya Mwendapole | Kuna mkakati wa kituo ambao unafanywa ili kuzuia maudhi (lugha zisizofaa) kwa wamama wajawazito na kamati ya kituo imejadili wahusika. Aidha, elimu itolewe kwa wananchi juu ya huduma na kuwasilisha malalamiko. | Kamati ya afya ya kituo, watoa huduma na Serikali za Mtaa. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **2.** | Kukosekana kwa huduma ya usafiri wa dharura wa wagonjwa (Ambulance) kwa wakati pale inapohitajika katika vituo vya Kongowe, Mwendapole, Misugusugu na Vikawe | Kutoa elimu kwa wananchi juu ya huduma ya usafiri wa dharura (si mara zote itapatikana kwa sababu ya hitaji kubwa kwa wananchi). Kutumia njia mbadala ili kuokoa maisha ya wagonjwa badala ya kutegemea huduma hiyo pekee. | WAJA, Watoa huduma na wananchi | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **3.** | Uhaba wa wahudumu wa Afya kama vile Tabibu, Mfamasia, Mhasibu, Manesi, mtu wa mapokezi na Washauri nasaha katika vituo vya Kongowe, Mwendapole, Misugusugu na Vikawe | Wilaya ipo katika mchakato wa kuangalia uhitaji halisia wa watumishi wilayani ili kuweza kuchukua maamuzi ya kuomba pamoja na kuongeza watumishi pale panapohitajika. | Mganga mkuu wa halmaushiri ya Mji (TMO) kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji pamoja na Waganga wafawidhi | Novemba 2020-Machi 2021 |
| **4.** | Watu wenye mahitaji maalum wapewe msamaha wa gharama za matibabu na kipaumbele | Kuweka utaratibu wa kuwapa kipaumbele watu wenye mahitaji maalum kituoni. Kuhamasisha watu wenye mahitaji maalumu | Watu wenye mahitaji maalum, Waganga wafawidhi, | Kuanzia Novemba na kuendelea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | katika kupata huduma yaani kuwa na Dirisha maalumu la huduma. | kujiunga na Bima ya afya (CHF) kwa gharama ya 30,000/=. Pia, kuhamasisha wadau waweze kusaidia watu wenye mahitaji maalum hususani wasiojiweza. | kamati za afya za vituo, Halmashauri na wadau | |
| **5.** | Kuboresha huduma za matibabu kwa watu wenye mahitaji maalum hasa upatikanaji wa dawa za watu wenye ulemavu wa ngozi kama vile vifaa kinga Sunblock, suncream and spray. | Kuomba wadau ili wagharamie dawa za watu wenye ulemavu wa ngozi. Dawa hazipo kwenye bajeti ya vituo ya dawa muhimu (Essential Medicine). Hivyo, Wadau wengine waungane na Halmashauri katika kusaidia watu wenye ulemavu wa ngozi. Waganga wafawidhi waandae bajeti ya dawa za ngozi kwa walemavu angalau chupa 3-5 (kwa sababu dawa za walemavu wa ngozi ni gharama zaidi). Takwimu za watu wenye ulemavu zipatikane ili bajeti iandaliwe kulingana na uhitaji. | Wadau, Halmashauri, Mganga mfawidhi. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **6.** | Hakuna Kipimo cha X-Ray katika Kituo cha afya Mkoani na Zahanati ya Kongowe | Jengo la huduma za X-Ray limesha jengwa na kwa sasa Kituo cha Afya kipo kwenye mpango wa kuleta kipimo cha X-Ray. Pia, elimu itolewe kwa wananchi juu ya upatikanaji wa kipimo cha X-Ray katika ngazi ya juu kuanzia kituo cha afya. | Mganga mfawidhi, Wajumbe wa kamati ya kituo na Halmashauri | Kuanzia Oktoba-Machi 2021 |
| **7.** | Ukosefu wa elimu ya matumizi ya dawa hasa kwa Walemavu. Dawa hazitolewi kulingana na maelekezo na ulemavu wa mtu kama ulemavu wa macho na masikio. Changamoto hii imeonekana katika Kituo cha afya Mkoani | Wagonjwa wenye mahitaji maalumu waje na ndugu ambao wanaweza kupokea maelekezo ya dawa vizuri badala ya kuja na watoto ambao hawawezi kupokea maelekezo vizuri. Watoa dawa watoe maelezo juu ya matumizi ya dawa kwa alama (Jua, mwezi nk) hususani kwa wagonjwa wenye mahitaji maalum kama wasiosikia (Viziwi). | Watoa huduma vituoni na wafamasia. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **8.** | Baadhi ya miundombinu sio mizuri na rafiki inahitaji kuboreshwa. Mfano; Njia ya kutoka | Changamoto ya barabara kutoka mapokezi kwenda maabara ifanyiwe kazi na wadau kwa kushirikiana na Halmashauri. | Wadau, Halmashauri, Mganga mfawidhi na | Kuanzia Oktoba-Machi 2021 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | mapokezi kwenda maabara ni mbovu. Vile vile, tenki la kuhifadhia maji halitoshi katika Kituo cha afya Mkoani. Pia, mifereji ya maji si misafi na kuna vichaka katika mazingira ya Kituo cha afya. | Tenki la kuhifadhia maji liwekwe/linunuliwe kwa bajeti za kituo na kuingizwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, Suala la usafi katika mazingira ya kituo cha afya lifanyiwe kazi ikiwezekana watu wa Magereza washirikishwe kama walivyokuwa wakishirikishwa kipindi cha nyuma. Wajumbe wa Kamati ya kituo walifanyie kazi mapema. | wajumbe wa kamati ya kituo. | |
| **9.** | Hakuna samani (furniture) za kutosha kukalia wagonjwa na wahudumu vituoni kama viti. Pia kuna uhaba wa makabati ya kuhifadhia kumbukumbu za wagonjwa. | Mganga mfawidhi aandae bajeti na kuipeleka kwenye Halmashauri kwa ajili ya kupata Samani. | Mganga mfawidhi na Mganga Mkuu wa Halmashauri | Kuanzia Oktoba-Machi bajeti inapoandaliwa |
| **10.** | Hakuna vyandarua kwa wanajamii wote zaidi ni walengwa tu kama Wamama wajawazito na watoto wa miezi 9 | Kugawa vyandarua kupitia wadau na kuhamasisha wananchi kununua vyandarua. | Halmashauri, Watoa huduma na WAJA | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **11.** | Baadhi ya WAJA hawapewi posho kutokana na kukosekana kwa mfumo rasmi wa malipo ya WAJA, hivyo kuathiri utoaji wa huduma kwa jamii. | Kuna mchakato wa kuweka mfumo rasmi ambao wadau watatumia ili kuweka fedha mfuko mmoja (pool) kwa ajili ya kuwalipa WAJA. | Halmashauri, Mganga mfawidhi | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **12.** | Uchache wa WAJA kwa baadhi ya mitaa ambao wanasaidia kuibua kesi za wagonjwa UKIMWI, Kifua kikuu nk) kama Misugusugu, Mwendapole na Vikawe | Kuhamasisha wananchi katika serikali za mitaa ili kuweza kujitolea kufanya kazi za WAJA. Wadau wanapokuja kuwatumia WAJA wapate taarifa/maelezo katika ngazi ya Halmashauri (H/shauri ihusishwe) | Waganga wafawidhi na wajumbe wa kamati za vituo na wananchi. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **13.** | Kichomea taka kinahitaji marekebisho madogo (Zahanati ya Visiga) | Bajeti ya ukarabati wa kichomea taka ijumuishwe kwenye bajeti ya kituo kwa mwaka wa fedha 2021/22 | Mganga mfawidhi na kamati ya afya ya kituo. | Novemba mpaka Machi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **14.** | Uhaba wa vifaa tiba kama vile Mabomba ya sindano ya chanjo ya BCG pamoja na TT, DPT na Surua. (Zahanati ya Visiga) | Halmashauri kuendelea kufuatilia upatikanaji wa mabomba kitengo cha chanjo Wizarani yaani EPI. | Halmashauri na Mganga mfawidhi na Serikali kuu | Wameshaanza kulishughulikia. |
| **15.** | Uhaba wa vitendea kazi kwa WAJA kama vile vitambulisho, mabegi, miamvuli, viatu vya mvua (gumboot), koti katika vituo vya Visiga, Kongowe na Vikawe. | Kupata msaada kutoka kwa wadau ili WAJA waweze kupata motisha ya vifaa vya kutendea kazi. Wadau wapitie ngazi ya Halmashauri ili kupata maelezo zaidi ya kuweza kuwawezesha WAJA. | Wadau, Halmashauri, Kamati za vituo na Jamii. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **16.** | Ukosefu wa nyumba ya mganga karibu na eneo la kituo ili kutoa huduma za dharura kwa urahisi katika vituo vya Kongowe na Vikawe | Kuibua miradi na kupeleka kwenye Serikali ya Mtaa/kata. Mikakati ianzishwe ya ujenzi wa nyumba za waganga/watumishi katika mitaa yetu kwa nguvu ya wananchi na kushirikisha ofisi ya Mkurugenzi & Mwandisi. | Serikali za mitaa, Waganga wafawidhi, Kamati za afya za vituo na wananchi | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **17.** | Kituo kipandishwe ngazi (hadhi) na kuwa Kituo cha afya kutokana na wingi wa wapokea huduma. Kituo kipo katikati (centre) na kinapaswa kuwa Kituo cha afya. | Zahanati ya Vikawe bado haijafikia hadhi ya kuwa kituo cha afya kwa sababu ya vigezo vya kupandisha zahanati kuwa kituo cha afya. Hata hivyo, kuna mchakato unaendelea kwa ajili ya kuhudumia jamii kubwa ya eneo la Kidimu na kwa sasa eneo linatafutwa kwa ajili ya kujenga Zahanati ili kuhudumia jamii ya Kidimu. | Serikali za mitaa pamoja na Halmashauri. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **18.** | Ukosefu wa jengo la wodi ya wazazi zahanati ya Misugusugu na Visiga | Changamoto inafanyiwa kazi kwani upanuaji wa zahanati ni kipaumbele katika Kata na muhtasari wa mradi ulishapitiwa katika ngazi ya Kata. Baadhi ya vifaa vimeanza kupatikana kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la wodi ya Wazazi. Hitaji la bajeti lipelekwe kwenye ngazi ya Halmashauri. Kwa upande wa Visiga, ujenzi wa wodi ya wazazi unaendelea na kwa sasa ujenzi wa wodi upo kwenye msingi kupitia fedha za | Mganga Mfawidhi, Wajumbe wa WADC, Kamati ya afya ya kituo, Idara ya Afya ya Halmashauri na jamii. | Kuanzia Novemba na kuendelea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | WADC. Aidha, ujenzi wa chumba cha kufungia vidonda unaendelea. | | |
| **19.** | Wazee wapewe kipaumbele kwenye huduma za afya katika ngazi ya Rufaa | Suala la Wazee kupewa kipaumbele kwenye huduma za afya katika ngazi ya Rufaa litafanyiwa kazi na Timu Afya Mkoa kwa kuwa Hospitali ya Rufaa ipo chini ya Mkoa. | Timu ya Usimamizi wa Afya Mkoani (RHMT) | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **20.** | Hitaji la mafunzo endelevu (Refresher course) kwa wajumbe wa kamati ya kituo pale inapohitajika | Kutoa mafunzo endelevu juu ya miongozo kwa wajumbe wa kamati za vituo. Wajumbe kuanisha maeneo wanayohitaji kupatiwa mafunzo na kuwasilisha kwa walezi wa vituo katika CHMT. | CHMT, Kamati ya kituo, Wajumbe wa kamati za vituo. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **21.** | Bima ya CHF iliyoboreshwa kutokidhi mahitaji ya walengwa kwani baadhi ya wanufaika hawapati dawa ambazo wameandikiwa. | Inawezekana dawa kwa wakati husika hazipo (haimaanishi hazipo kabisa), hivyo wagonjwa wanaweza kuzitafuta kituo kingine. Pia hamasa/Elimu itolewe kwa watu wengi wajiunge na CHF iliyoboreshwa ili watu wengi wapate mahitaji ya dawa. | WAJA, watoa huduma, Wajumbe wa Kamati za vituo | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **22.** | Elimu bado ndogo kwa baadhi ya wananchi juu ya upatikanaji/kujiunga na Bima ya afya | Kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wananchi pia WAJA kupata elimu zaidi ili kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kujiunga na CHF iliyoboreshwa. | Wananchi, WAJA, Wajumbe wa kamati ya Kituo | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **23.** | Muda ni mchache katika utoaji wa huduma mwisho saa 10 jioni katika Zahanati ya Misugusugu na Kongowe. | Wananchi wapewe elimu kwamba Zahanati haitoi huduma masaa 24. Pia kuna namba ya simu kwa ajili ya huduma za dharura kituoni. | WAJA, Watoa huduma kwenye kituo pamoja na wananchi. | Kuanzia Novemba na kuendelea |
| **24.** | Kukosekana kwa umeme mbadala hasa umeme unapokosekana/kukatika hivyo kuathiri utoaji wa huduma. | Kituo kiandae bajeti na kuipa kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji | Mganga mfawidhi wa Kituo, Mwenyekiti wa kamati ya kituo na Jamii kuhusika | Kuanzia Oktoba-Machi 2021 |
| **25.** | Huduma kuchelewa kuanza katika clinic ya watoto na wajawazito, | Kituo kinafanyia kazi changamoto hii ambayo hutokana na uhaba | Mganga mfawidhi na | Kuanzia Oktoba mpaka Januari 2021 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ambapo huduma za upimaji huanza kutolewa kuanzia saa 3 hadi 4 asubuhi, hivyo kusababisha mrundikano wa wateja. | wa watumishi kituoni pamoja na likizo kwa watumishi. | kamati ya afya ya kituo | |
| **26.** | Uhaba wa dawa za kuharisha. | Dawa zipo ila ni suala la kuendelea kuelimisha watu juu ya dawa mbadala au zilizopo. | Watoa huduma, WAJA na jamii husika. | Kuanzia Novemba na kuendelea |

***Kiambatanisho Na 2: Orodha ya washiriki***

| No. | Kundi la Uwakilishi | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Wapokea Huduma (Jamii)** | | | | |
| **1.** | Watu wenye ulemavu | 4 | 4 | 8 |
| **2.** | Watu waishio na VVU/UKIMWI (WAVIU) | 17 | 9 | 26 |
| **3.** | Wagonjwa wa kifua kikuu (TB) | 7 | 9 | 16 |
| **4.** | Vikundi vya wanawake | 13 | - | 13 |
| **5.** | Vijana | 7 | 4 | 11 |
| **6.** | Wanawake wajawazito | 6 | 0 | 6 |

| No. | Kundi la Uwakilishi | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Vyombo vya Usimamizi wa Huduma za Afya na WAJA** | | | | |
| **1.** | Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (WAJA) | 16 | 27 | 43 |
| **2.** | Wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa vituo vya kutolea Huduma za Afya | 15 | 13 | 28 |
| **3.** | Viongozi wa Kijamii | 9 | 6 | 15 |
| **4.** | CHMT | 7 | 6 | 13 |
| **5.** | RHMT | - | 1 | 1 |

| No. | Kundi la Uwakilishi | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Vyombo vya Usimamizi wa Huduma za Afya** | | | | |
| **1.** | Kituo vya Afya | 3 | 1 | 4 |
| **2.** | Zahanati | 7 | 7 | 14 |

**Sikika inafanya kazi ya kuhimiza uboreshaji wa mifumo ya afya na usimamizi wa fedha kupitia uwajibikaji jamii na uraghibishi katika ngazi zote za serikali**


Barabara ya Haile Salassie,
Mtaa wa wa Mwaya, Masaki
Nyumba Na. 1387C,
S.L.P 12183, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 222 26 580 15

Ujumbe mfupi: 0688 493 882
Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz,
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika1
Instagram: Sikika1

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani,
S.L.P 1970 Dodoma, Tanzania.
Simu: 0262321307
Nukushi: 0262321316